

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF FINANCE**



MILLENNIUM CHALLENGE ACCOUNT – TANZANIA

**KAMPUNI YA H. YOUNG & CO. (E.A) LTD KUJENGA BARABARA
TANO (5) ZA MKOA WA KASKAZINI PEMBA KWA KIWANGO CHA
LAMI CHINI YA MPANGO WA MCA-T**

Tarehe 18 Agosti Millennium Challenge Account-Tanzania (MCA-T), ikiwa na jukumu la kusimamia utekeleaji wa miradi inayopata fedha kutoka serikali ya Marekani kupitia Shirka la Millennium Challenge Corporation (MCC), imesaini mkataba wa Tsh 38, 247,730,180.00 na kampuni ya M/S H Young & Co.(E.A) Ltd kwa ajili ya kuanza kazi za kujenga barabara tano (5) za Kaskazini Pemba kwa kiwango cha lami. Kazi hii itafanyika kwa kipindi cha miezi 18 na inatarajia kuanza mara moja. Barabara hizo tano (5) zenye jumla ya urefu wa km 35 ni:-

- i. Barabara ya Mzambarauni Takao Pandani Finya yenye km 7.9
- ii. Barabara ya Mzambarauni Karimu Mapofu yenye km 8.7
- iii. Barabara ya Bahanansa Daya Mtambwe yenye km13.8
- iv. Barabara ya Chwale Road yenye km 1.9. na
- v. Barabara ya Kipangani Kangagani yenye km 2.7

Sherehe za utiaji saini mkataba huo zimefanyika Wete Pemba na kuhudhuriwa na viongozi wa serikali, taasisi za kiraia, dini na wananchi kutoka maeneo ya mradi.

Akizungumza wakati wa sherehe hiyo, Afisa Mtendaji Mkuu wa MCA-T, Mr. Bernard Mchomvu ameipongeza kampuni ya H Young kwa kushinda zabuni hii kupitia mchakato mkali na wa ushinadani, aliwataka waifanye kazi hiyo kitaalam na kwa muda uliopangwa “Ni matarajio yetu mtatekeleza wajibu wenu kwa ufanisi katika maeneo husika na kwa muda uliopangwa” alisisitiza Mr. Mchomvu

Pia Mr. Mchomvu alitoa taarifa kuwa maandalizi yote ya kazi hiyo yamekamiliika ikiwemo kuwalipa wananchi wapatao 1,7,28 ambao nyumba zao zitabomolewa kupisha ujenzi wa barabara. Hadi sasa jumla ya Tshs 3.9 billion zimetumika kuwalipa wananchi hao. Aidha, alieleza kuwa kazi ya ujenzi wa barabara hizi utafanyika chini ya usimamizi wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kampuni ya /s LEA Associates Consultancy, ambayo ni mhandisi mshauri itasimamia shughuli za ujenzi za kila siku..

Afisa Mtendaji Mkuu wa M/S H Young Mr Joseph Schwartzman alishukuru kwa kushinda zabuni hii na kuahidi kutekeleza yote yaliyomo kwenye makataba na kwamba atashirikiana na wadau wote katika kufanikisha kazi hii.

Uboreshaji wa barabara hizi unatarajia kuleta manufaa makubwa kwa wakazi wa mkoa wa Kaskazini Pemba ikiwemo kurahisisha usafirishaji wa mazao, kukuza kipato cha mwananchi, kuboresha mawasiliano, kuvutia watalii na kurahisisha upatikanaji wa huduma za jamii kama elimu na afya.

Ujenzi wa barabara za Pemba kwa kiwango cha lami ni moja ya miradi ya sekta ya usafirishaji inayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano chini ya msaada wa dola za kimarekani milioni 698.1 zilizosainiwa na Mhe. George W. Bush aliyekuwa Rais wa Marekani na Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, February 17, 2008 katika Ikulu ya Dar es Salaam ili kuchochea ukuaji uchumi. Miradi mingine ni ile ya sekta ya umeme na maji.



Mr Bernard Mchomvu (kushoto) and Mr Joseph Schwartzman (kulia) wakisaini mkataba wakiwa wanashuhudiwa na Mhe. Alfonso Lenhardt (wa tatu kulia), Balozi wa Marekani nchini; Mhe. Hamad Masoud Hamad (wa tatu kushoto), Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano- Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; Mr. Karl Fichenscher (wa kwanza kushoto); Mkurugenzi Mkazi wa MCC; Mr. Khamis M. Omar (wa pili kushoto), Katibu Mkuu Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango - Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; Mr. Omar Khamis Othman (wa pili kulia), Mkuu wa Wilaya ya Wete kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Wete na Mr. Antony Kimani (wa kwanza kulia) kutoka H.Young &Co (E.A) Ltd

####

Millennium Challenge Account-Tanzania (MCA-T) is an autonomous and independent Government Entity established to implement a \$698 million grant that will reduce poverty by improving infrastructure and thereby promoting economic growth. MCA-T is supported by Millennium Challenge Corporation (MCC), a United States government agency designed to work with developing countries. For more information visit www.mca-t.go.tz or www.mcc.gov.